



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

**WIZARA YA HABARI, MAWASILIANO NA
TEKNOLOJIA YA HABARI**

**MWONGOZO MDOGO WA UTOAJI WA NAMBARI ZA
ANWANI ZA MAKAZI**

Februari, 2022

1.0 UTANGULIZI

Mwongozo huu mdogo ni ufafanuzi wa Mwongozo Mkuu wa Anwani za Makazi wa Mwaka 2016. Mwongozo huu wa Utoaji wa Nambari za Anwani umeandaliwa ili kumsadia mtoaji wa Nambari za Anwani katika Mitaa/Shehia/Vitongoji aweze kutoa namba kwa usahihi kulinga na melekezo, Sheria, Kanuni na Taratibu zilizopo.

2.0 WATUMIAJI WA MWONGOZO

Mwongozo huu utatumiwa na Mkoa/Wilaya/Halmashauri ili kupata uelewa wa namna ya kutoa nambari za Anwani za makazi katika maeneo yao. Pia mwongozo huu utatumiwa na Afisa /Mtaalamu/ Mtu yeyote atakayeteuliwa na kuidhinishwa na Katibu Tawala wa Mkoa au Mkurugenzi wa Halmashauri husika kutoa nambari za Anwani katika Mtaa/Shehia/Kitongoji husika.

4.0 UTARATIBU WA UTOAJI WA NAMBARI ZA ANWANI

i. Nambari za Nyumba

Nambari za nyumba zinapaswa kuendana na vigezo vilivyobainishwa katika mwongozo huu. Nambari hizo wakati wote zinapaswa zionekane kwa uwazi kutoka pande zote za barabara. Aidha, mambo yafuatayo yazingatiwe:

- a. Ziwe katika rangi inayojitofautisha na mandhari yake ya nyuma; kibao chenye rangi ya njano kiwe na maandishi meusi kama ilivyoelekezwa kwenye Kiambatisho 'D'; na
- b. Kibao cha nambari ya nyumba kiwe na urefu usiopungua inchi nne (4) na upana usiozidi inchi kumi (10), isipokuwa pale ambapo mmiliki ameomba kutumia nambari kubwa zaidi.

ii. Muundo na Mwanzo wa Utoaji Nambari

a. Muundo wa Nambari

Nambari ziwe katika mfumo rasmi wa nambari za Kiarabu (Kwa mfano 1, 2, 3, ...);

b. Mwanzo wa utoaji wa nambari za Anwani .

Nambari za Anwani zitatolewa kuanzia Mwanzo wa barabara au njia inayoingia katika mtaa/shehia husika. Kwa kawaida mwanzo wa barabara au njia unaweza kuwa:

- i. Katikati ya Mji Pointi ya Kilometa Sifuri “Zero Kilometre” pale ambapo barabara kuu za mji husika zinapoanzia kuelekea nje ya Mji; au
- ii. Mwanzo wa barabara kutoka katika makutano ya Barabara Kuu na barabara/ mtaa/njia inayotakiwa kupewa nambari. Kigezo hiki kitatumika endapo katika makatano hayo kuna mji/kituo cha biashara kikubwa zaidi ya kule ambako barabara inaeneleka (katikati ya mji). Au
- iii. Kama itakavyoamuliwa na kupangwa na Mamlaka za Serikali za Mitaa ambazo hupanga mwanzo na mwisho wa barabara au njia na hivyo ramani zitumike wakati wa utoaji wa nambari.

5.0 UGAWAJI WA NAMBARI

a. Ugawaji wa Nambari za Anwani katika maeneo ya Mijini

Nambari za Anwani katika maeneo ya mijini zitagawiwa kwa mfuatano wa nambari witiri kwa upande wa kushoto wa barabara na nambari shufwa kwa upande wa kulia wa barabara kuanzia mwanzo wa barabara katika mtaa husika. Nambari tofauti ya Anwani ya mtaa itapaswa kugawiwa kwa kila eneo la nyumba/kiwanj. Hakutakuwa na nambari moja itakayogawiwa ikiwa ni uendelezaji wa makazi ya mjini. (Rejea Mchoro ufuatao)




b. Ufafaunuzi wa Ugawaji Nambari


Pamoja na melezo hayo vielelezo vifuatavyo vinafafanua namna bora ya kugawa namba katika mitaa/shehia/vitongoji

- i. Kugawa namba kwenye nyumba zinazotegemea Barabara Kuu na barabara za Mitaa katika maeneo yaliyopangika, nambari zitagawiwa kwa mfuatano wa namba witiri au shufwa kutegema upande barabara kuanzia mwanzo hadi mwiso.


Aidha katika mazingira ambapo kiwanja kimoja kina jengo zaidi ya moja, nambari zitagawiwa kwa mfuatano wa namba witiri au shufwa kutegema upande barabara kwa kutoa nambari moja ya anwani katika jengo kuu (Anwani kuu) na majengo mengine yatapelewa nambari ya Anwani Kuu kwa kuongeza kiambishi cha herufi mwishoni mwa nambari hiyo, Mfano Anwani Kuu ni 1, Anwani tegemezi ni 1A, 1B, 1C. (Rejea mchoro ufuatao)




- ii. Kwa anwani zilizopo katika duara, nambari zitagawiwa kwa mfuatano wa nambari witiri au shufwa kutegema upande barabara kuanzia mwanzo wa mtaa.;



- iii. Katika maeneo ambapo kuna barabara inayounganisha Mikoa miwili, kila Mkoa utatoa nambari za Anwani kutoka mwanzo wa barabara kama ilivyoa ainishwa katika mwongozo huu.
- iv. Ugawaji wa nambari za anwani katika barabara moja yenye jina lile lile inayokatisha kutoka Wilaya moja kwenda Wilaya nyingine ndani ndani ya Mkoa, bila kujali kama miji imeungana au haijaungana, nambari za anwani zitagawiwa kwa muendelezo wa nambari kutoka Wilaya moja hadi nyingine kwa kuzingatia mwanzo wa barabara na upande wa barabara. (Rejea mchoro Ufuatao)-



- v. Endapo kuna barabara kuu inayounganisha mikoa miwili na katikati ya hiyo Mikoa kuna Makao Makuu ya Mkoa mwingine ambayo hayajapitiwa na barabara kuu, utoaji wa nambari za Anwani katika barabara hiyo (Barabara Kuu ambayo haijapita kaitikati ya Makao Makuu ya Mkoa) utanzia upande ambao barabara inayoingia katika Makao Makuu ya Mkoa huo ipo karibu zaidi na mpaka wa Mkoa wa upande mmojawapo. (Rejea Mchoro Ufuatao)



- vi. Utoaji wa nambari za Anwani katika jengo ambalo lina milango katika mtaa zaidi ya mmoja; jengo hilo litapewa nambari katika upande wa barabara ambapo lango kuu la kuingilia katika jengo hilo linatazama. (Rejea Mchoro Ufuatao).




- vii. Utoaji wa nambari za Anwani katika maeneo (Mitaa) ya Mijini yaliyojengwa bila kuzingatia mipango miji. Nambari za Anwani zitatolewa kwa muendelezo wa nambari witiri au shufwa kulingana na upande wa barabara kuanzia mwanzo wa barabara.

Aidha, endapo viwanja vitakuwa havijaendelezwa katika eneo linalogawiwa nambari, basi hifadhi ya nambari ifanyike kwa ajili kugawa baada ya ujenzi kukamilika. (Rejea Mchoro ufuatao).



- viii. Nambari za Anwani katika maeneo ya vijijini zitagawiwa kwa utaratibu usio wa mpangilio kama maeneo yaliyopangwa. Utaratibu utakaotumika ni kutoa namba za anwani kwa mfuatano wa namba kuanzi 1,2,3,4,.....




- ix. Utoaji wa Anwani kwa Maduka Makubwa ya Biashara
 Maduka Makubwa ya Biashara yatapelewa nambari moja ya anwani ya mtaa iliyotolewa kwa mtaa unaounganisha lango kuu la magari. Nambari tofauti za anwani hazipaswi kutolewa kwa kila lango la maduka makubwa ya biashara. (Rejea Michoro Ifuatayo)



- x. Utoaji wa Nambari katika Nyumba zilizotenganishwa
 Anwani za nyumba zilizotenganishwa zitagawiwa kwa mfuatano wa nambari witiri katika upande wa kushoto na nambari shufwa katika upande wa kulia wa barabara au mtaa.


- xi. Anwani za makazi katika maeneo hatarishi/ yaliyozuiliwa
Mpango wa utoaji wa Anwani za makazi hautahusisha maeneo hatarishi/
yasiyoruhusiwa kwa makazi mfano: mabondeni, kwenye vyanzo vya maji,
maeneo oevu, maeneo ya hifadhi, maeneo ya wazi na maeneo ya hifadhi ya
barabara isipokuwa katika maeneo maalum tu yaliyoruhusiwa.




KIAMBATISHO 'D'

UAINISHO WA VIBAO VYA NAMBARI ZA NYUMBA D1 - Uainisho wa kitaalamu wa Vibao vya nambari ya nyumba

Na	Maelezo	Ukubwa	M f a n o (Kibao cha Nambari y a Nyumba)	M f a n o (K i b a o c h a Nambari y a Nyumba)	Maunzi
1	<p>Kibao cha nambari Kibao cha nambari ya nyumba cha rangi ya njano chenye ufito mweusi na m a a n d i s h i meusi.</p>	<p>U k u b w a wa kibao Tarakimu ikiwa moja Upana wa mm 100 X unene wa mm 4 X urefu wa mm 125</p>		3	Plastiki angavu nyeupe
	<p>Kila kibao LAZIMA kiwe na matundu ya kufunga kwa skrubu ili kubana katika ukuta pembeni mwa mlango wa mbele.</p>	<p>T a r a k i m u z i k i w a mbili Upana wa mm 180 X unene wa mm 4 X urefu wa mm 125</p>		36	Plastiki angavu nyeupe
2	<p>Kila kibao cha nambari ya nyumba LAZIMA kiwe na skrubu mbili (2) zitakazofungwa katika plagi z i l i z o p o ukutani.</p>	<p>N a m b a r i tatu Upana wa mm 250 X unene wa mm 4 X urefu wa mm 125</p>		136	Plastiki angavu nyeupe

Na	Maelezo	Ukubwa	M f a n o (Kibao cha Nambari y a Nyumba)	M f a n o (K i b a o c h a Nambari y a Nyumba)	Maunzi
3	<p>Ukubwa wa Maandishi Ukubwa wa maadishi utategemea ukubwa wa kibao</p> <p>Ufito Ufito wa pembeni kuzunguka maandishi</p>	<p>Si chini ya upana wa mm 76 X urefu wa mm 100</p> <p>U f i t o mweusi Takriban mm 4 k u t o k a k a t i k a ukingo wa kibao</p>			



D2 - Maelekezo ya Uwekaji wa Vibao vya Nambari za Nyumba

Ukubwa wa kibao cha nambari ya nyumba	Kibao chenye tarakimu Moja	Kibao chenye tarakimu Mbili au Tatu
Ufito	Ufito mweusi wa pembeni kuzunguka maandishi	Ufito mweusi wa pembeni kuzunguka maandishi
Mwelekeo	Wima	Mlalo
Aina ya maandishi	Maandishi makubwa ya mviringo na yaliyokolezwa ('Arial Rounded MT Bold')	Maandishi makubwa ya mviringo na yaliyokolezwa ('Arial Rounded MT Bold')
Ukubwa wa Maandishi	Takribani urefu wa mm 100 X upana wa mm 76	Takribani urefu wa mm 100 X upana wa mm 76
Unene wa kibao	mm 4	mm 4
Uwekaji wa Skrubu na plagi	Mshazari au wima	Mshazari au mlalo
Mahali sahihi pa kuweka kibao	Kibao kitawekwa katika ukuta upande wa kulia wa mlango wa mbele au kwenye mlango	Kibao kitawekwa katika ukuta upande wa kulia wa mlango wa mbele au kwenye mlango.

D3- Njia mbadala za uandishi wa nambari za nyumba

Pale ambapo Mkurugenzi wa Halmashauri ataona inafaa nambari za nyumba zitaandikwa katika milango au ikilazimu ukutani kwa wino mweusi kama ilivyoelezwa katika D1. Mazingira yanayoweza kumfanya Mkurugenzi wa Halmashauri kufikia maamuzi hayo ni kama ifuatavyo:-

- i. Maeneo ya vijijini;
- ii. Makazi yasiyopangwa; na
- iii. Maeneo ya watu wanaohamama.

